

JIELIMISHE KUHUSU UGONJWA WA HOMA KALI YA MAPAFU UNAOSABABISHWA NA KIRUSI CHA CORONA

DALILI



Homa na Mafua Makali



Kikohozi



Kubanwa mbavu na
kupumua kwa shida



Mwili Kuchoka



Maumivu ya Misuli




Vidonda kooni



Kuumwa Kichwa


JINSI YA KUJIKINGA



Nawa mikono kwa maji



Funika mdomo na pua



Kaa mbali na mtu mwenye mafua au kikohozi ambaye
ana historia ya kusafiri nje ya nchi

Funika mdomo na
pua wakati wa
kukohoa au kupiga
chafya kwa kitambaa
safi au sehemu ya
mbele ya kiwiko cha
mkono



JKINGE NA WAKINGE WENGINE DHIDI YA MAGONJWA

Nawa mikono yako kwa maji tiririka na sabuni:



- **Baada ya kukohoa au kupiga chafya**
- **Baada ya kumhudumia mgonjwa**
- **Kabla na baada ya kuandaa chakula**
- **Kabla ya kula**
- **Baada ya kutoka chooni**
- **Baada ya kushika mnyama au kinyesi cha mnyama**

Ugonjwa wa homa ya kirusi cha Corona unatibika?

Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja, hivyo kama yalivyo magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi, matibabu hufanyika kwa kuzingatia dalili zilizopo na ufuatiliaji wa karibu.



Je, ni salama kupokea barua, kifurushi au mzigo toka nchi zenye mlipuko wa ugonjwa wa Corona?

Ndiyo ni salama. Mtu hawezi kuambukizwa virusi vya Corona kwa njia ya kupokea barua, vifurushi au mzigo kutoka nchi zilizokumbwa na ugonjwa huo.

Virusi vya Corona haviishi kwa muda mrefu kwenye vitu kama barua, vifurushi au mizigo.

